

## **Athari za mlipuko wa ugonjwa wa KORONA kwa afua za kuthibiti malaria, idadi ya wagonjwa na vifo barani Afrika: uchambuzi wa kijiografia**

### **Muhtasari**

#### **Utangulizi**

Kumekuwa na hatua kubwa katika kupunguza kiwango cha ugonjwa wa malaria katika bara la Afrika tangu mwaka 2000. Hata hivyo, mafanikio hayo yanaweza kuathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa KORONA (COVID-19) iwapo utaathiri upatikanaji wa afua za kudhibiti malaria. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini mabadiliko yanayoweza kutokea kwenye idadi ya wagonjwa na vifo vitokanavyo na malaria kutokana na kuathirika kwa afua za kudhibiti malaria.

#### **Mbinu za utafiti**

Uchambuzi wa taarifa kwa kutumia mbinu za kitakwimu zinazohusisha maeneo ya kijiografia na nyakati, umeweza kukadiria viwango vya wagonjwa na vifo vitokanavyo na malaria kwa nchi zote za Afrika zinazoathiriwa na ugonjwa huu, kwa kujumuisha taarifa za tafiti juu ya ukubwa wa maambukizo, uwepo wa vyandarua vyenye viutilifu, na ufanisi katika tiba ya wagonjwa. Tumefanya makadirio kabla ya mlipuko wa KORONA na baada kutokea kwa mlipuko kwa kuangalia mazingira tofauti tisa ya kuathirika kwa ufanisi katika matibabu na upatikanaji wa vyandarua.

#### **Matokeo**

Tumekadiria jumla ya wagonjwa milioni 215.2 (95% kiwango cha usahihi 143.7–311.6) na vifo elfu 386.4 (307.8–497.8) kwa nchi zote zinazoathiriwa na malaria katika bara la Afrika kwa mwaka 2020 kabla ya mlipuko wa KORONA (kabla afua za kudhibiti malaria hazijaathirika). Kwa kupungua kwa upatikanaji wa tiba sahihi dhidi ya malaria, utafiti wetu umekadiria ongezeko la wagonjwa milioni 224.1 (148.7–326.8) na vifo elfu 487.9 (385.3–634.6) kwa upungufu wa 25% kwenye ufanisi wa matibabu; wagonjwa milioni 233.1 (153.7–342.5) na vifo elfu 597.4 (468.0–784.4) kwa upungufu wa 50%; na wagonjwa milioni 242.3 (158.7–358.8) na vifo elfu 715.2 (556.4–947.9) kwa upungufu wa 75%. Kusitisha kampeni za usambazaji wa vyandarua kwa jamii zilizopangwa kwa mwaka 2020 na kupunguza utoaji wa vyandarua kupitia taratibu zingine kwa asilimia 25–75 pia imeongeza wagonjwa wa malaria kwa milioni 230.5 (151.6–343.3) na vifo elfu 411.7 (322.8–545.5) kwa kushuka kwa 25%; wagonjwa milioni 232.8 (152.3–345.9) na vifo elfu 415.5 (324.3–549.4) kwa kushuka kwa 50%; na wagonjwa milioni 234.0 (152.9–348.4) na vifo elfu 417.6 (325.5–553.1) kwa kushuka kwa 75%. Kushuka kwa pamoja kwa upatikanaji wa vyandarua na ufanisi katika tiba kumeongeza wagonjwa wa malaria kufikia milioni 240.5 (156.5–358.2) na vifo elfu 520.9 (404.1–691.9) kwa upungufu wa 25%; wagonjwa milioni 251.0 (162.2–377.0) na vifo elfu 640.2 (492.0–856.7) upungufu wa 50%; na wagonjwa milioni 261.6 (167.7–396.8) na vifo elfu 768.6 (586.1–1038.7) kwa upungufu wa 75%.

#### **Ufafanuzi**

Kuathirika kwa juu kabisa katika afua za kudhibiti malaria kunakoweza kuletwa na KORONA barani Afrika kunaweza kuongeza maradufu vifo vitokanavyo na malaria katika mwaka 2020. Kuna uwezekano wa kuwa na ongezeko kubwa zaidi katika miaka inayofuata. Kuepusha kurudi nyuma kwa matokeo makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miongo miwili iliyopita katika juhudi za kupambana na malaria, ni vema kuendelea kuipa kipaumbele mikakati iliyowekwa na kuendelea kuitekeleza kwa mjumuisho na ile inayolenga kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa KORONA.

#### **Ufadhili**

Mfuko wa Bill na Melinda Gates; Channel 7 Telethon Trust, Western Australia.